



My new preschool

Shule yangu mpya ya mapema



Picha zote katika waraka huu zinamilikiwa na Idara ya Elimu ya NSW chini ya Sheria ya Kaimiliki 1968 (Copyright Act 1968 (Cth)) au zina leseni chini ya iStock [Getty Images Content License Agreement](#)

Hili ndilo lango la kuingia shule yangu mpya ya mapema.



Nina begi la shule ya mapema ambalo hubeba mgongoni mwangu. Ninaliweka mahali maalum ninapofika kwa shule ya mapema.



Ninachukua sanduku la chakula cha mchana na chupa cha maji kwa shule ya mapema. Nikiwa na kiu najipatia maji ya kunywa.



Nina kofia ya kuva kwa shule ya mapema.
Ninavaa wakati ninapocheza nje kunikinga na juu



Watu wazima katika shule yangu ya mapema wanabitunza na kenisaidia kujifunza. Nawaambia ninapokuwa na huzuni na wanenisaidia kujisikia vizuri zaidi. Watu wazima wale wanakumbusha kila mtu kuwa marufiki wema.



Nina marafiki wengine wa zamani ambao nacheza nao kwa shule ya mapema, na marafiki wengine wapya pia. Siku nyingine, lakini, najisikia kucheza peke yangu.



Kuna vitu vingi tofauti vyatya kucheza navyo kwa shule ya mapema. Kila siku nachagua kile ninachotaka kufanya. Napenda kujifurahisha na kujifunza vitu vipyta.



Wakati ninapocheza ndani, napenda kutengeneza vitu kwa kutumia karatasi na masanduku. Nikikuwa na huzuni, natengeneza na bloku vizuizi, kama vile mimi ninavyofanya nyumbani.



Wakati ninapocheza nje, napenda kukimbia na kupanda juu ya vifaa. Napenda pia kucheza na mchanga.



Wakati wa kucheza unapokamilika, mimi husaidia kupakia vitu vya kuchezea. Ni vizuri kutunza shule yetu ya mapema na kuiweka nadhifu.



Mara mwingine, watoto na watu wazima wanakutana pamoja ili kujifunza vitu vipyta na kuimba nyimbo. Tunafurahia pia kushiriki hadithi pamoja, kama mimi ninavyofanya nyumbani.



Wakati pua yangu imejaa, napata karatasi na kupiga chafya. Baada ya kumaliza, nakumbuka kuweka karatasi kwenye pipa la kuosha mikono yangu.



Kuna chumba kikubwa cha bafu katika shule yangu ya mapema. Naingia chumba hiki wakati ninapohitaji kutumia choo. Halafu nikimaliza, naosha choo na kuosha mikono.



Naosha mikono yangu na sabuni na maji na kisha hukausha. Ninafaa sana kukumbuka kunawa mikono yangu. Ninahakikisha ninaosha vijidudu vyote ili niwe na afya.



Nakula chakula changu cha mchana pamoja na watoto wengine. Ikiwa siwezi kufungua chakula changu, naomba msaada wa mtu mzima. Kila mara mimi hula chakula changu chote chenye afya ili niwe na nguvu na afya njema. Ikiwa sitakula chakula changu chote, nafunga kile kilichobaki na kwenda nacho nyumbani.



Baada ya tumekula chakula cha mchana, ni wakati wa utulivu. Watoto wote hufanya kitu kimya, kama kuangalia kitabu, mafumbo au kuchora. Wakati wowote mwili wangu unapochoka, mimi hulala chini na kupumzika.



Wakati unakaribia kufika nyumbani, nafunga begi langu na kuiweka mgongoni, kuwa tayari kwenda nyumbani.



Mwishoni wa siku ya mapema, watoto wote wana mtu mzima anayekuja kuwasindikiza nyumbani.



Ninapoondoka, ninatabasamu na kusema kwa heri kwa watu wazima na watoto. Nasema, “Asante kwa kucheza, tukutane wakati mwingine.” Wakati kila mtu ameondoka, shule yangu ya mapema inafungwa.

